

# Notisi ya Kutobagua na Ufikikaji

Legacy inazingatia sheria zinazohusika za haki za raia za Serikali na haibagui kwa misingi ya umri, asili, kabila, utambulisho wa jinsia, dini, mwelekeo wa kijinsia, elimu, hali ya kustaafu kutoka kwa jeshi, ulemavu, historia ya mtu ya kijamii na kiuchumi, au sifa nyingine yoyote.

Wagonjwa hupokea kiwango sawa cha utunzaji na ufikivu wa huduma, bila kujali au kuzingatia umri, asili, kabila, jinsia, dini, mwelekeo wa kijinsia, elimu, ulemavu, historia ya mtu ya kijamii na kiuchumi, au sifa nyingine yoyote.

Wagonjwa wana haki ya kupata habari kuhusu jinsi wanavyotunzwa na kutibiwa kwa njia na muundo unaotilia maanani umri, lugha, na uwezo wao wa kuelewa. Kwa kuzingatia sheria za Haki za Raia, Sheria ya Waamerika wenye Ulemavu (Americans with Disabilities Act) na Tume ya Pamoja (The Joint Commission), Legacy hutoa njia iliyo bora zaidi ya kuwasiliana na wagonjwa.

Legacy hutoa huduma za lugha bila malipo kwa wale ambao Kiingereza sio lugha yao ya kwanza, huduma za ukalimani zinapatikana katika kila idara ya shirika hili. Legacy huarifu wahudumu wote kuhusu upatikanaji wa huduma za ukalimani na huwezesha wagonjwa na familia kuwasilisha mahitaji na matakwa yao.

Legacy huajiri wakalimani wanaozungumza Kihispania katika hospitali na kliniki za Legacy Good Samaritan na Legacy Emanuel na hutoa kandarasi za huduma za ukalimani katika maeneo yote ambapo huduma za Legacy zinapatikana ili kufasiri taarifa (maneno yanayosemwa au maandishi) katika lugha tofauti na kwa watu wenye ulemavu wa kusikia. Sera ya Legacy, Interpreters for Hearing Impaired and Non-English Speaking Patients (Huduma ya Ukalimani Kwa Wagonjwa wenye Ulemavu wa Kusikia na Wale Wasiozungumza Kiingereza) (100.32), inafafanua michakato ya kufikia wakalimani.

Legacy hutoa vifaa vya usaidizi na huduma kwa watu wenye ulemavu ili kuwawezesha kuwasiliana nasi kwa njia iliyo bora zaidi, kama vile:

- Wafasiri wa lugha ya ishara waliohitimu
- Taarifa zilizoandikwa kwa mfumo wa kielektroniki
- Simu za TTY

Mtu yeyote anayehitaji vifaa vya usaidizi au huduma za lugha anaweza kuomba kupata huduma kutoka kwa mfanyakazi yeyote wa Legacy.

Mtu yeyote anayeamini kwamba Legacy imekosa kutoa huduma hizi ama imembagua kwa njia yoyote ile kwa misingi ya asili, rangi, taifa la asili, umri, ulemavu, jinsia au utambulisho wa kijinsia, anaweza kuwasilisha malalamishi kwa Idara ya Uzingatiji ya Legacy kwa:

- Kupiga simu kwa laini ya moja kwa moja kupitia 1-800-820-7478
- Kutoa ripoti mtandaoni kupitia <https://www.reportlineweb.com/legacyhealth>
- Kutuma barua pepe kwa [compliancofficer@lhs.org](mailto:compliancofficer@lhs.org)

Unaweza pia kuwasilisha malalamishi ya ukiukaji wa haki za kiraia kwa Idara ya Afya na Huduma za Kibinadamu, Ofisi ya Haki za Raia (U.S. Department of Health and Human Services, Office for Civil Rights), kwa njia ya kielektroniki kupitia Tovuti ya Ofisi ya Malalamishi ya Haki za Kiraia, inayopatikana katika <https://ocrportal.hhs.gov/ocr/portal/lobby.jsf>, au kupitia barua au simu kwa:

U.S. Department of Health and Human Services (Idara ya Afya na Huduma za Kibinadamu)  
200 Independence Avenue, SW  
Room 509F, HHH Building  
Washington, D.C. 20201  
1-800-868-1019, 800-537-7697 (TDD)

Fomu za Malalamishi zinapatikana katika <http://www.hhs.gov/ocr/office/file/index.html>

